GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXIII Nam. 6484 **8 Julai, 2013** **Bei Shs. 15,000/=**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti *Hutolewa kila Ijumaa*

YALIYOMO *Ukurasa*

Mswada wa Sheria wa Kurekebisha Sheria
mbali mbali za Ardhi na mambo yanayohusiana
na hayo..... 243

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Mswada uliyotajwa hapo chini umetangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili

Tangazo la Mswada

Nam. :- Mswada wa Sheria Kurekebisha Sheria mbali mbali za Ardhi.

T A N G A Z O

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanza tarehe 12 Juni, 2013 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

ZANZIBAR
8 Julai, 2013

(Dkt. ABDULHAMID Y. MZEE)
Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

MSWADA
wa

SHERIA YA KUREKEBISHA SHERIA MBALI MBALI ZA ARDHI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

IMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi Zanzibar

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Jina fupi na tarehe ya kuanza kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya marekebisho ya Sheria mbali ya 2013 na itaanza kutumika mara tu baada ya kutiwa Saini na Rais.

Kusomwa.

2. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Umilikaji Ardhi Nam. 12 ya 1992 ambapo katika Sheria hii itajulikana kama "Sheria Mama".

SEHEMU YA PILI
MAREKEBISHO YA SHERIA YA UMILIKAJI ARDHI NAM. 12 YA 1992.

Marekebisho ya kifungu cha 2.

3. Kifungu cha 2 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kuongeza tafsiri mpya kwa mpangilio wake wa kiherufi kama ifuatavyo:-

"Taasisi ya Serikali" maana yake ni Wizara, Idara za Wizara naWakala, Shirika la Serikali,Mamlaka ya Serikali, Tume, Bodi ya Serikali, Kampuni ambayo ianamilikiwa na Serikali ikiwa na hisa nyingi".

Marekebisho ya kifungu cha 8.

4. Kifungu cha 8 (1) cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kufuta na kuandikwa upya aya (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(b) "Kwamba mwenye kudhibiti maslahi ya taasisi ya Serikali, au kampuni, au washiriki wa biashara ambao wenye hisa nyingi ni Wazanzibari au Jumuiya za kiraia.

Kwa madhumuni ya kifungu hiki Jumuiya za kiraia maana yake ni Jumuiya za kiraia ambazo zimesajiliwa Zanzibar, zinafanya shughuli zake ndani ya Zanzibar na wanachama wake ni Wazanzibari tu.

(c) "Mzanzibar yoyote ambae alikua ana sifa ya kuwa mzanzibar na akapoteza sifa hizo atakuwa na haki zifuatazo:-

(i) Kurithi ardhi iliyokuwa inamilikiwa na mtu ambae alikuwa na haki ya kisheria kumrithi.

(ii) Kupata ardhi ambayo alikuwa akimiliki kihalali kabla ya kukosa sifa ya kuwa Mzanzibar.

(iii) Kupata ardhi kwa njia ya hiba kwa mtu ambaye wanauhusiano wa damu.

5. Kifungu cha 56 cha sheria mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:- Marekebisho ya kifungu cha 56.

(b) "Kwa wale waliopata kutoka kwa Waziri, kupata haki nyengine ya umiliki kwa ardhi yoyote iliyochukuliwa na kulipwa fidia kwa maendeleo yaliyofanywa katika ardhi hio".

2. Kuongeza aya mpya za (c) na (d) kama ifuatavyo:-

(c) "Kwa kulipa fidia yenye kuridhisha ya ardhi pamoja na gharama za maendeleo yaliyofanywa katika ardhi hio"

(d) "Kwa haki nyengine ya umiliki wa ardhi, kulipa fidia yenye kuridhisha kwa kuzingatia thamani ya ardhi pamona na harama za maendeleo yaliyofanywa katika ardhi hiyo".

SEHEMU YA TATU
MAREKEBISHO YA SHERIA YA USAJILI WA ARDHI NAM. 10 YA 1990

6. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usajili wa Ardhi Nam. 10 ya 1990 ambapo katika sheria hii itajulikana kama sheria mama. Kusomwa.

MADHUMUNI NA SABABU.

Madhumuni ya Mswada huu ni kupendekeza marekebisho ya Sheria mbali mbali nazo ni:-

i. Sheria ya Umilikaji Ardhi Nam. 12 ya 1992

ii. Sheria ya Usajili wa Ardhi Nam. 10 ya 1990 Mswada umegawika katika sehemu kuu tatu.

Sehemu ya kwanza ni utangulizi ambapo inaeleza jina fupi na kuanza kutumika kwa Sheria zinazopendekezwa. Vile vile inaeleza kusomwa sambamba kwa Sheria inayopendekezwa na Sheria ya Umilikaji Ardhi Nam. 12 ya 1992.

Sehemu ya pili inahusiana na marekebisho ya Sheria ya Umilikaji Ardhi Nam. 12 ya 1992 ambayo inafanyiwa marekebisho yafuatayo:-

Kifungu cha 3 kinahusu marekebisho ya kifungu cha 2 ambapo inapendekezwa kuongeza tafsiri ya maneno mapya.

Kifungu cha 4 kinahusu marekebisho ya kifungu cha 8 (1) ambapo inapendekeza kufutwa na kuandikwa upya kwa aya (b) na (c)

Lengo la marekebisho hayo ni kuruhusu Taasisi za Serikali, Jumuiya za kiraia au Kampuni kupata haki ya matumizi ya ardhi. Vile vile kuweka utaratibu wa kupata haki kwa Mzanzibar ambaye alikuwa na sifa ya kuwa Mzanzibar na baadae akapoteza sifa hiyo.

Kifungu cha 5 kinahusu marekebisho ya kifungu cha 56 ambapo kinapendekeza kufuta na kuandikwa upya kwa aya (b) pamoja na kuongezwa aya mpya ya (c) na (d).

Lengo la marekebisho hayo ni kuweka tofauti ya fidia baina ya wale waliopewa haki ya matumizi kwa kununua, kurithi au hiba na wale ambao wamepata kutoka Serikalini, kwa wale ambao wamepewa haki hiyo na Serekali kwa kuwalipa ada ndogo tu ambapo Serikali itahitaji eneo husika kwa matumizi mengineyo, Serikali iweze kulichukuwa eneo hilo kwa kumpa eneo jengine mbadala pamoja na kumlipa fidia ya maendeleo yaliyofanyika, au kumlipa fidia stahiki kwa ardhi hiyo pamoja na maendelezo yaliyofanyika.

Sehemu tatu inakusudia kufanya marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Ardhi Nam. 10 ya 1990 ambayo inafanyiwa marekebisho kwa kufuta kifungu cha 36 36(1) na kuvipa namba upya badala ya zilizokuwepo.

Lengo la marekebisho ni kulilinda rejista dhidi ya uharibifu wa aina zote. Kifungu hiki kinatoa nafasi kwa mtu yeyote anaetaka kulikagua rejista kufanya hivyo baada ya kujaza fomu na kulipa ada iliyowekwa.

ZANZIBAR (RAMADHAN ABDULLA SHAABAN)
8 Julai, 2013 ***Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati***